Wapishi wa wanafunzi na wapishi wa Sodexo Wilayani kote wakati wa Mashindano ya Wapishi wa Siku za Baadaye katika PCTA Jumatano, Machi 18.

MIUNGANISHO

MACHI, TAREHE 31, 2023

KONA YA AFISA MKUU MSIMAMIZI

DKT. JAVIER MONTAÑEZ
MSIMAMIZI MKUU

Karibu kwenye toleo jipya la Shule ya Umma ya Wilaya ya Providence (PPSD) kijarida cha mara mbili kwa wiki! Ikiwa wewe au mtu unayemjua atakosa mojawapo ya vijarida vyetu, unaweza kupata matoleo ya awali kwenye tovuti ya Wilaya katika lugha nyingi.

Wiki iliyopita, nilitembelea **Mount Pleasant High School** pamoja na **Mayor Brett Smiley**. Niliweza kupata muda na wanafunzi na wafanyakazi kupata maoni kuhusu shule yao na Wilaya. Wanafunzi wanaendelea kunivutia wakati wa mazungumzo. Meya pia alivutiwa na alipokea karibisho changamfu kutoka kwa wafanyakazi na wanafunzi.

Pia napata msisimko kiasi wakati baridi inaanza kupungua na siku inaanza kuwa ndefu. Wakati wa masika, tunaona dunia kwa mtazamo mpya wakati miti inaanza kutoa maua. Ni muda pia ambapo wanafunzi wetu wanaonyesha ubora wao --wakati wanafunzi wetu wa shule za sekondari wanashiriki orodha yao ya kukubaliwa chuoni, mipingo ya kujitolea kwa jeshi na mipango ya biashara. Wako na tumaini na ndoto ambazo bila shaka zina sisimua jumuiya ya shule.

Tuko na talanta ya kipekee Wilayani kote. Hakikisha kutazama **Mashindano ya Sodexo ya Mpishi wa Siku za Baadaye** hapo chini. Nangoja kwa hamu siku moja kujaribu mchanganyiko wa parachichi unaotengenezwa na Shawn Andrews wa Carnevale. Kulingana na majaji na wapishi wa Sodexo, wanafunzi wote walioshiriki walitengeneza milo bora.

Hivi karibuni shule zetu zitakuwa kwa likizo. Tunafurahia ya kwamba zaidi ya wanafunzi 2000 wetu watashiriki katika **Academia ya Likizo ya Masika** wakati wa wiki hiyo. Tunafurahi kuwashirikisha kwa fursa za masomo za furaha, na uzoefu wa moja kwa moja kuwasaidia kujitayarisha kwa mitihani ya RICAS na SAT. Tunatumaini wanafunzi wetu wote na wafanyakazi wanafurahia likizo ya masika walio stahiki.

WEKA ALAMA KWA KALENDA YAKO!

- **IJUMAA KUU (HAKUNA SHULE)**
  Ijumaa, Aprili 7
- **AKADEMIA YA LIKIZO YA MASIKA**
  Jumatatu, Aprili 10 - Ijumaa, Aprili 14
  saa tatu asubuhi 9:00 a.m hadi saa saba mchana 1:00 p.m.
- **MAPUMZIKO YA MAJIRA YA MASIKA**
  Jumatatu, Aprili 10 - Ijumaa, Aprili 14
- **USAMBAZAJI WA CHAKULA BILA MALIPO**
  Jumanne, Tarehe 11 Aprili, saa nne asubuhi 10:00 a.m.
  Asa Messer, Feinstein katika Broad, DelSesto, Gilbert Stuart, Nathanael Greene, Roger Williams

APRILI MENYU YA SHULE

TAARIFA MPYA ZA WILAYA

TAREHE YA SURVEYWORKS IMESONGESHWA

Siku ya mwisho kwa wazazi wote wa Rhode Island kujaza fomu ya maoni ya kila mwaka ya utafiti wa **SurveyWorks** imesongeshwa hadi Ijumaa, Aprili tarehe 7. Tafadhali tembelea www.RIDE.ri.gov/SurveyWorks kabla ya Aprili tarehe 7. Inachukua dakika 20 tu kukamilisha utafiti huo katika kompyuta, simu bapa au kifaa cha mkononi. Wazazi wa wanafunzi wa PPSD wanaweza kutembelea kiungo hapo juu, au kutafuta ujumbe wa maandishi kutoka shule yako na kutoka kwa Wilaya kwa kutumia msimbo wa QR ambao unaweza kutambaza. Sauti yako ni muhimu kwetu na tunashukuru maoni yako!

MEI TAREHE 17 USASISHO WA KALENDA

Tafadhali tambua kwamba katika kalenda zenu **Jumatano, Mei tarehe 17** imebadilishwa kuwa siku kamili ya shule badala ya siku ya kuachiliwa mapema. Hakutakuwa na siku ya kuachiliwa mapema kwa maendeleo ya kitaaluma wakati wa mwezi wa Mei.

UKUMBUSHO WA MAPUMZIKO YA MAJIRA YA MASIKA

Ukumbusho kwa wanafunzi wote wa PPSD na familia zao ya kwamba mapumziko ya majira ya masika itaanza Jumatatu, tarehe 10 Aprili hadi tarehe 14 Aprili. Madarasa yatarudi tena mnamo Jumatatu, tarehe 17, Aprili. Sodexo itaandaa usambazaji wa chakula bila malipo Jumanne, tarehe 11 Aprili kuanzia saa nne asubuhi 10:00 a.m katika shule sita. **Asa Messer, Feinstein katika Broad Street, DelSesto, Gilbert Stuart, Nathanael Greene,** na **Roger Williams**. Tunatumaini utakuwa na likizo ya Aprili nzuri na ya kupumzika.

AKADEMIA YA MAPUMZIKO YA MAJIRA YA MASIKA

Tunafurahi kuwa na wanafunzi zaidi ya 2,000 walio sajili katika **Akademia ya Mapumziko ya Majira ya Masika** ya PPSD hadi sasa! Bado kuna muda kwa familia za wanafunzi katika madarasa ya 3-5, darasa la 8, na darasa la 11 kusajili katika Akademia inayofanyika wakati wa mapumziko ya majira ya masika (Jumatatu, tarehe 10 Aprili-Ijumaa, tarehe 14 Aprili) kuanzia saa tatu asubuhi 9:00 a.m hadi saa saba mchana 1:00 p.m. Jiunge nasi kwa wiki ya furaha na masomo ya moja kwa moja katika hisabati, sayansi, na kusoma. Sajili kwa shule ya mtoto wako au hapa: https://www.providenceschools.org/SpringBreakAcademy

USAWA KWA FURSA KATIKA SHULE ZA UMMA ZA PROVIDENCE

MANENO YAKO NA NGUVU

Wale ambao wanafanya kazi kwa kutafuta usawa, utofauti, na kushiriki duniani kote, watashuhudia kwamba kazi inaweza kuwa ya manufaa sana na yenye changamoto ya kupendeza. Hii kwa sababu kazi yetu mara nyingi inapeana changamoto kwa maadili na imani zetu ambazo tume beba tangu zamani. Kwa binadamu wengine, changamoto hizi zinaweza kusababisha mawazo ya ndani, ubadilishaji wa imani za muda mrefu na utengenezaji wa maadili mapya. Kwa wengine, utokeaji wa hisia za woga na wasiwasi unaweza sababisha uchaguzi mbaya na utumizi wa maneno ya kudhalilisha. Ni lazima tukumbuke kwamba ingawa tunaweza kutokubaliana, uchaguzi wa maneno yetu ni muhimu. Vijana wetu wanatazama. Tazama blogu hii kutoka Sauti za Vijana wa UNICEF.

MACHI TAREHE 31 NI SIKU YA MWONEKANO WA WABADLLISHA JINSIA!

Siku ya Mwonekano wa Wabadllisha Jinsia (SMWJ) ina tambulika duniani kama siku ya kuleta ufahamu kuhusu na kusherekea watu walio badilisha jinsia. Pia ni siku ya kujenga ufahamu kuhusu ubaguzi na kutokuwa sawa ambao watu walio badilisha jinsia hupitia, na hata pia ustahimilivu wao na nguvu ya kuishi kihalisi.

PPSD inajivunia kuwa na Sera ya Kutobagua kwa Walio badilisha Jinsia na wanafunzi Wenye Jinsia Pana, na hata pia Sera ya Kazini ya Mpito wa Jinsia kwa wafanyakazi. Tafadhali tazama tovuti ya Usawa na Ushiriki katika providenceschools.org/equity kwa rasilimali kusaidia na kuunga mkono walio badilisha jinsia na wanafunzi na wafanyakazi wenye jinsia pana. Mwongozo kuhusu kusasisha taarifa ya mwanafunzi inapatikana hapa pia.

KUANGAZIA MWEZI WA HISTORIA YA WANAWAKE:

REBECCA KISLAK ni wakili mwenye uzoefu, mtaalamu wa sera, mzazi wa PPSD na Mwakilishi wa Jimbo la Rhode Island. Kupitia uongozi wake wa bodi na wa kitaalamu, ameonyesha ufanisi katika utengenezaji wa mahusiano, wakili wa ushirikiano, uendelezo wa mpango, uwezeshaji na mkakati wa mpangilio. Ni mshiriki aliyejitolea na anaye shughulika katika Kamati ya Ushauri wa Usawa na ana tetea kwa dhati kanuni na sera za usawa jimboni kote na kwa viwango vya wilaya.

I'LANNI BURGOS ni mwanafunzi wa darasa la nane anaye hudhuria **Esek Hopkins Middle School** na ni mmoja wetu wa Shujaa wa Usawa Wilayani. Anafurahia kuhudhuria Classical High School wakati wa msimu wa vuli ambapo anatarajia kwa hamu kuchunguza taaluma tofauti. Anapendezwa na ubunifu wa ndani, sheria na falaki. Hivi majuzi amependezwa na Ujenzi wa Ndani katika RISD na ana chunguza uchaguzi tofauti wa shule za sheria. Wakati wa kutembelea kilele cha uongozi wa vijana na safari ya majuzi ya Wiki ya Haki ya Kijamii, Angie amekuwa mshiriki amilifu wa kudumu na mshirika wa jumuiya mwenye mfano bora.

BI. KRYSTAL LOFTON ni mmoja wapo wa shujaa wengi katika Wilaya yetu. Ametengeneza nafasi na muda kwa Ofisi ya Usawa na Ushirikiano kupeana maendeleo ya kitaalamu kwa Walimu wakuu wasaidizi, wanao lenga kuongoza kwa usawa na ufahamu wa ubaguzi wa rangi. Bi. Lofton anaamini kwamba ni jukumu lake kuhakikisha tuna viongozi wa "sasa hivi" ambao wanazingatia utamaduni na hawa choki kusukuma mabadiliko ambayo yana boresha kufundisha na kusoma na yana pendekeza usawa.



XARIS ni kijana anaye jiunga na **Alvarez High School** na ni mmoja wa mashujaa wa usawa Wilayani kote. Xaris ana uwezo maalum wa kupata kilicho bora kutoka kwa wanafunzi wenzake bila kuzingatia utofauti wa kitamaduni ambao uko. Wenzake na walimu wakati wanapo ongea kuhusu Xaris husema, "kila mara atapatikana kukusaidia na kufanya jambo bora litoke kwako." Ni kiongozi mkimya na mwenye ujasiri anaye shawishi mawazo na vitendo vya wengine katika jumuiya yake. Xaris ana hamu ya kusoma na amejitolea kutengeneza mabadiliko.

AMY HARRINGTON ni mtaalamu wa Kusoma na Kuandika kwa Middle School na mwalimu mkongwe. Amejitolea kusaidia walimu katika vitendo vyao vya kuangazia utamaduni kufikia kila mwanafunzi. Kama mtetezi, Amy ana wezesha wale walio karibu naye kuangazia na kukomesha mapendeleo. Asante, Amy, kwa kuwa bingwa wa usawa.

ANGIE MICHEL ni shujaa hodari wa usawa, kiongozi wa wanafunzi na mfano bora kwa wanafunzi wenzake. Angie alichaguliwa kama raisi wa wanafunzi katika **Nathan Bishop Middle School**, na amekuwa akivutia kila mtu kwa ujuzi wake wa kipekee wa uongozi tangu wakati huo. Kama raisi wa wanafunzi, Angie amechukua majukumu kadhaa, ikiwemo kusimamia operesheni za serikali ya wanafunzi, kuwakilisha jopo la wanafunzi katika kamati tofauti na kuwakilisha nia za wanafunzi. Anaonyesha mfano wa kiongozi bora, ambaye anasikiliza, anaheshimu na ana thamini mitazamo ya wengine. Angie ni raisi wa wanafunzi bora na chanzo cha matumaini kwa wenzake. Mafanikio yake ya kipekee kwa uongozi na kwa masomo yameweka kiwango cha juu kwa wengine kufuatilia, na ameweza kujithibitisha kuwa rasilimali ya thamani katika jumuiya ya wanafunzi.

KUWASHEREHEKEA WANAFUNZI

Wanafunzi wetu wenye bidii na wenye talanta wanafanya mambo mazuri kila siku. Hapa kuna mifano michache.

CENTRAL E-SPORTS IMEENDA KWA NAFASI YA KWANZA

Hongera kwa **timu ya E-Sports ya Central High School** kwa ushindi wao dhidi ya Ponaganset! Ushindi huu ulifunga Central katika nafasi ya kwanza! Hongera kwa **Dasani Silva** kwa kuwa Mchezaji wa Thamani Zaidi, na timu yote kupata ushindi kwa Knights. Kazi nzuri sana, na bahati njema katika msimu wote!

MASHINDANO YA SODEXO PROVIDENCE YA MPISHI WA BAADAYE

Hongera kwa mwanafunzi wa darasa la nne **Shawn Andrews** kutoka **Anthony Carnevale Elementary School** kwa kutajwa kuwa Mshindi wa Mashindano ya Sodexo Providence ya Mpishi wa Siku za Baadaye! Mlo wa ushindi wa Shawn ulivutia sana jopo la majaji, ikiwemo mwanafunzi wa Classical wa mwaka wa pili chuoni kikuu, Lynnaly Luciano, mshindi wa Mpishi wa Siku za Baadaye wa mwaka 2018, mwanabodi wa PPSD Tyrell Stephens, na Johnson & Wales Assoc. Profesa Michael Makuch, MAT, CEC. Hongera kwa **Veazie Street Elementary School , Savannah Villegas** kupata nafasi ya pili kwa ushindi. Wanafunzi walishinda zawadi nzuri ikiwemo vitabu vya upishi na vyombo vipya vya upishi! Watarajiwa wote wapishi vijana walifanya vyema sana katika mashindano, na wanapaswa wajivunia sana mafanikio yao.

SIKU YA NJAA KUU YA KIWAVI

Wanafunzi wa shule ya chekechea katika **Asa Messer Elementary School** walisherekea "Siku ya Njaa kuu ya Kiwavi" kwa kusoma kitabu cha watoto kinacho pendwa kilicho andikwa na Eric Carle. Wanafunzi walitengeneza kofia za viwavi na sanaa zingine tofauti kusaidia kusherekea siku hiyo! Kila mtu alikuwa na furaha sana kusoma kitabu hicho na kushiriki katika sanaa na ufundi!



NATHANAEL GREENE ANANG'ARA

"Kuwa na ndoto, na usikubali mtu yeyote aichukue," alisema Msimamizi mkuu Montañez Ed.D. wakati wa matembezi katika **Nathanael Greene Middle School** kuongea na wanafunzi, walimu na wasimamizi. Aliongea na darasa kuhusu umuhimu wa elimu na kufuata ndoto zao. Alihimiza wanafunzi kuja shuleni na "kujipatia fursa bora zaidi kwa maisha bora."

KUANGAZIA WANAFUNZI WAKUBWA

Pata kufahamu wanafunzi wetu wakubwa hodari Wilayani!

Kutana na wanafunzi wakubwa kutoka Classical, Carmen na Hector ambao wote walikubaliwa katika MIT

Carmen Boyan
Mwanafunzi mkubwa, Classical High School
ES: Henry Barnard Elementary katika RIC
MS: Bishop Middle School

Hector Flores
Mwanafunzi mkubwa, Classical High School
ES: Lauro & West Elementary
MS: Nathanael Greene Middle School

Mipango yako ni gani baada ya shule ya sekondari?

CB: Nili ingia katika Stanford hatua ya mapema. Pia niliingia katika MIT na Chuo Kikuu cha Chicago. Bado nangoja kusikia kutoka Harvard na Columbia. Napenda sana mchanganyiko wa wasomi wakuu na wachezaji hodari, pamoja na hali ya anga ya joto katika Stanford. Nili wasilisha ombi katika shule sita kwa ujumla. Nilishangaa sana kuingia kwa baadhi za shule ambazo niliingia.

Napenda sayansi, lakini sijui ni kwa sehemu gani ya sayansi. Niko na uzoefu na jenitikia. Nilijifunza kazi katika Chuo kikuu cha Brown wakati wa msimu wa kiangazi uliopita ambayo ilikuwa katika jenomiki ya kompyuta, ambayo ni kama mchanganyiko kati ya jenitikia pamoja na sayansi ya kompyuta. Lakini napendelea pia sayansi ya neva, ambayo ilitengenezwa wakati wa darasa langu la AP Saikolojia. Pia sayansi ya mazingira, ambayo ilinivutia katika Stanford. Labda nitaingia kwa utafiti au jambo kama hilo, sina uhakika.

> "Classical ni kama huleta kila mtu kutoka sehemu tofauti. Haijalishi unatoka wapi, hadi pale unaonyesha unaweza kufanya kazi kwa bidii."

Nyinyi nyote mumeingia MIT? Je, hilo lilikuwa lengo lako daima?

HF: Kwa hakika ili tishia—mchakato wote wa usajili—kwa hivyo nili wasilisha ombi kwa shule nyingi kuwa salama. Nili wasilisha ombi kwa shule 18. Tuko na upunguzaji wa ada ya shule, kwa hivyo tunafanya iwe rahisi kuwasilisha ombi kwa shule nyingi, hiyo na Programu ya Jumla. Shule zangu za kiwango cha juu zilikuwa MIT, Harvard na Brown. Lakini nili jitoa kutoka shule za Ligi ya Ivy baada ya kusajiliwa katika MIT. Uchaguzi wangu wa pili ulikuwa WPI. MIT ilikuwa shule yangu ya ndoto, na nimechunguza shule hii na binamu wangu mara kadhaa kabla ya kuingia na baada ya kuingia.

Ninapendelea sehemu ya robotiki. Mimi sio wa hapa; nimetoka Mexico wakati nilipokuwa darasa la kwanza. Nilifanya mpango wa ESL katika shule ya msingi. Sababu nimetaja hiyo ni kwa sababu babu yangu ndiye aliyenileta kwa sayansi. Alinifundisha muunganisho wa waya wa msingi na kulehemu kufanya nianze eletroniki.

Shughuli zako za mtaala ziada ni gani?

CB: Katika miaka nne kwa Classical, nimecheza voliboli na lakrosi. Pia nafanya kukwea mawe ambayo inafurahisha sana, klabu cha hispania na klabu cha usawa wa kijinsia. Pia nacheza zeze na piano.

HF: Nilifanya bendi miaka nne yote. Nilicheza tarumbeta. Wakati nilipokuja hapa, hakukuwa na klabu rasmi cha robotiki. Rafiki yangu alitaka nianzishe, kwa hivyo nilifanya kazi naye kuanzisha. Tulianza kutafuta ufadhili na ufadhili nje na tuka pitia makala haya na jinsi Brown alitaka kupanua robotiki katika shule za sekondari. Tuliwasilia profesa katika Chuo kikuu cha Brown na tukapata vifaa. Ilikuwa mwanzo wa pole pole kwanza kwa sababu ya COVID, lakini wakati wa mwaka wa vijana ilishika kasi tena.

Ni mfanyakazi gani amekuwa na athari kubwa kwako?

CB: Bi. Hickey na Bw. Harding. Bi. Hickey pia ni mkufunzi wangu wa uwanja wa hoki, na nilikuwa kwa darasa lake la mwaka wa kwanza na mwaka wa pili chuoni. Daima alikuwa akinipa changamoto. Ako na sifa dhabiti ambayo inafurahisha kuwa karibu naye. Bw. Harding ni mshauri wa mwongozo. Yeye ni bora zaidi, na atafanya chochote kwa yeyote yule.

HF: Tangu siku ya kwanza, mshauri wangu wa mwongozo, Bw. Verecchia, alitaka kuni fahamu. Ilisaidia kufahamu ni nini ninachotaka kufanya tangu mwanzoni. Anapenda kusema jinsi nilimtafuta wakati wa kiangazi wakati wa mwaka wangu wa nane kwa sababu nilimpigia simu kujifunza zaidi kuhusu uchagunzi wa AP shuleni. Alijitolea kukutana nami shuleni, alitambua niko na maono makuu, aliona kwamba nimejitolea kwa kazi yangu, na akanisaidia katika masomo yangu ya AP. Aliona uwezo wangu. Ni vitendo hivi vidogo ambavyo vinafanya kuwa hakika kuna watu ambao wanakutakia mema na wanataka upate mafanikio.

Je, uli jifunza nini ukiwa shule ya sekondari?

CB: Nadhani kutengeneza marafiki na kufanya kazi na wengine kujaribu kuelewa vitu ilikuwa fundisho kubwa. Kama katika fizikia mwaka uliopita, wengi kati yetu hatukuelewa dhana kwa hivyo tuli tembelea Chuo kikuu cha Brown, na kutumia ubao mweupe katika jengo lao, na kutatua shida zote. Kuna njia nyingi nilijifunza kufanya kazi na wengine wakati mambo hayakunijia kirahisi kwangu.

HF: Nadhani Classical ilinifunza kuthamini muda na bidaa ninayo fanya. Nakumbuka changamoto wakati wa miaka ya awali, wakati nakumbuka kupambana na changamoto nyingi kuzoea lugha. Classical ilinifundisha kuna kufanya kazi kwa bidii, na hakuna mambo mengi yatakayo kuja kwako bila bidii. Kwa hivyo unapaswa ufanye bidii kwa kazi zote. Hii ina thamani sana, kwa vile shule kama MIT inaweza kuwa na changamoto kuu.

Je, una shukuru kwa kutoka Shule za Providence?

CB: Mimi na rafiki yangu tuli toa hotuba katika maelekezo ya wanafunzi wa mwaka wa kwanza chuoni mwezi uliopita, na tuli ongea kuhusu jinsi tunajivunia kusema kwamba tuli enda Classical. Niko na Majivuno mengi ya Zambarau. Ni eneo la furaha.

HF: Nadhani utamaduni unaopatikana Classical na roho ya shule inakuja na mandharinyuma tofauti ambazo zinakuja pamoja hapa. Sote tuko na wakati mzuri. Nadhani ni mambo unayo pata katika shule za umma ambayo huwezi kuyapata katika shule za kibinafsi. Classical ni kama huleta kila mtu kutoka sehemu tofauti. Haijalishi unatoka wapi, hadi pale unaonyesha unaweza kufanya kazi kwa bidii.

WILAYANI



MAENDELEO YA UONGOZI WA MWALIMU MKUU MSAIDIZI WA PPSD

Walimu wakuu wasaidizi Wilayani kote wanahudhuria mpango wa mikakati ya maendeleo na uongozi hivi majuzi. Mpango huu unalenga kusaidia AP kuwa viongozi wa nguvu. "Funzo langu kuu ni uhusiano wa kirafiki na ushirikiano," alisema Jaime David, **Nathanael Greene Middle School** Mwalimu Mkuu msaidizi, "kufahamu kwamba sio mimi pekee mwenye hisia kama hizo. Ya kwamba sio mimi pekee ambaye anahitaji kiwango fulani cha usaidizi... Najifunza njia tofauti za kupanga uongozi wangu kwa njia ya ushirikiano na ya mafanikio." Asanteni nyote kwa AP hodari Wilayani!



MPANGO WA UFUNDISHAJI KAZI WA TEKNOLOJIA YA HABARI

Wanafunzi wa **PCTA CTE PTECH** wana fursa ya kujifunza kuhusu kompyuta na teknolojia ya habari kupitia ufundishaji kazi wa kulipwa Wilayani na maeneo ya biashara. Mpango wa ufundishaji kazi unaendelea katika PCTA na wanafanya kazi kuieneza hadi kwa shule zingine za CTE Wilayani. Wanafunzi wako na fursa kuingia ndani katika kiwanda cha taaluma na kupata uzoefu wa kufanya kazi moja kwa moja ndani ya sehemu hiyo kwa mapema. Jifunze zaidi kuhusu jinsi uzoefu huo umekuwa kwa wanafunzi na waajiri husika katika video hapa.

MAYOR SMILEY ANA TEMBELEA MOUNT PLEASANT

Asante kwa **Meya Brett Smiley** kwa kuja kutembelea **Mount Pleasant High School** kuongea na wanafunzi na walimu wetu. Meya pamoja na Msimamizi mkuu Dkt. Javier Montañez, walikuwa na matembezi katika shule ya sekondari, na walipata fursa ya kuongea na baadhi ya wanafunzi na wafanyakazi hodari, na hata kujifunza kuhusu uwekezaji unaofanyika shuleni. Asante kwa kutembelea, Meya Smiley!

MASHINDANO YA KUREMBESHA MLANGO

Wanafunzi katika **Gilbert Stuart Middle School** walifanya kazi pamoja kutengeneza ubunifu tofauti kuweka katika milango ya madarasa yao kama sehemu ya mashindano ya kurembesha mlango. Mada ya mashindano ilikuwa Jumuiya, na wanafunzi walikuja na njia tofauti za kujumuisha mada hiyo katika kazi ya sanaa yao. Kazi nzuri sana ya kushirikiana na wengine kutengeneza ubunifu bora wa milango!

NI HABARI NJEMA: PPSD KWENYE VYOMBO VYA HABARI

- Brown itapeana ufadhili wa masomo Kabla ya Chuo kwa wanafunzi wote walio sajiliwa katika shule za umma za Providence
  Habari za Brown, Februari tarehe 16
- Hope High Ina sherekea Gloria Patterson Katika Sifa Bora Zaidi
  Yurview, Machi13
- Mwanariadha wa shule ya sekondari ya Providence anashinda Tuzo la Gatorade la Mchezaji wa Mwaka
  WJAR, Machi tarehe 17
- Mjuzi wa Kazi Zote – Tyler Lee wa Classical
  WPRI, Machi tarehe 25

Mambo ya kusisimua yanatokea katika Wilaya nzima, na tunataka kueneza ujumbe! ikiwa una programu, hafla, mfanyakazi, au mwanafunzi mwenye hadithi nzuri ajabu ambayo ungependa kuonyesha, tafadhali tuma barua pepe kwa communications@ppsd.org.

Providence Schools

© 2023 Providence Public Schools · communications@ppsd.org · www.providenceschools.org